**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Nne – Tarehe 14 Disemba, 2022.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Kufuta Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar, Nam. 7 ya 1996 na Kuanzisha Mamlaka ya Mapato Zanzibar kama Chombo Kikuu cha Kufanya Tathmini na Kukusanya Mapato Yaliyoainishwa ili Kusimamia na kutekeleza Sheria Zinazosimamia Mapato Hayo na Mambo Mengine Yanayohusiana.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi Kuhusu Mswada wa Kufuta Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar, Nam. 7 ya 1996 na Kuanzisha Mamlaka ya Mapato Zanzibar kama Chombo Kikuu cha Kufanya Tathmini na Kukusanya Mapato Yaliyoainishwa ili Kusimamia na kutekeleza Sheria Zinazosimamia Mapato Hayo na Mambo Mengine Yanayohusiana.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

5. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

   Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuyatunza mazingira yetu na kupiga vita uharibifu wa aina tofauti dhidi ya

mazingira hayo, bado nchi yetu inakabiliwa na changamoto ya uharibifu wa mazingira.

Je, Serikali ina mpango na mkakati upi wa kuzuia uharibifu wa mazingira, hususan uchimbaji holela wa mchanga ndani ya makaazi yetu pamoja na ukataji wa miti kiholela.

<u>**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**</u>

80. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kuna baadhi ya watumishi wa Serikali wamehudumu katika utumishi wao kwa muda mrefu lakini bado hawajathibitishwa kazini hadi hivi sasa.

(a) Je, ni lini watumishi hao watathibitishwa.

(b) Je, ni athari gani za kimaslahi zitakazowakabili wafanyakazi wanaocheleweshwa kuthibitishwa baada ya kumaliza kazi.

108. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali inaamini kwamba, mfumo wa sheria na utoaji wa haki wenye ufanisi kwa nchi yoyote ile ni kitovu cha uchumi, ustawi wa jamii, amani na utulivu. Hata hivyo, tafiti zinaonesha kwamba, kunahitajika mageuzi makubwa na kuimarisha utekelezaji wa sheria na utoaji wa haki Zanzibar.

(a) Ni upi mpango wa Serikali katika kuleta mageuzi ya sekta ya utekelezaji wa sheria na utoaji wa haki mbali na kuimarisha majengo ya Mahkama pekee.

(b) Je, Serikali haioni haja na umuhimu wa kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar na kutoa Toleo Jipya la Sheria za Zanzibar [Revised Zanzibar Law Edition], ili kufuta rasmi Toleo la Sheria za Zanzibar la mwaka 1958 sambamba na kufanya mapitio ya huduma zinazojenga taaluma ya Sheria (Legal Education).

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

16. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika kuwasaidia wananchi wa Zanzibar, Serikali yetu inawaelekeza wawekezaji mbali mbali kushiriki katika maendeleo ya wananchi hasa waliowazunguka katika maeneo yao ya uwekezaji.

(a) Kwa kuwa katika jimbo la Mwanakwerekwe kuna wawekezaji mbali mbali wakiwemo wamiliki wa vituo vya kuuzia mafuta, benki na maghala, Je, Serikali imewahamasishaje na kuwaelekeza katika kuchangia miradi mbali mbali ya wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe.

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuwaelekeza wawekezaji hao kushiriki katika maendeleo ya wananchi mbali mbali wa jimbo la Mwanakwerekwe.

(c) Je, kwa kiwango gani utaratibu wa kuwashirikisha wawekezaji mbali mbali katika jimbo la Mwanakwerekwe umekuwa unatekelezwa ipasavyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

55. MHESHIMIWA PANYA ALI ABDALLA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato (Zan Malipo) kwa Taasisi zake. Suala la kusikitisha ni kuwa baadhi ya Taasisi zinashindwa kutumia mfumo huo kutokana na upungufu wa vitendea kazi.

Je, Serikali imejipangaje kuzipatia taasisi hizo vitendea kazi ili kutumia mfumo huo.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

29. MHESHIMIWA ABDULLA HUSSEIN KOMBO (Jimbo la Mkoani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naipongeza Wizara yako kwa kuamua na hatimae kukipatia meli ya uvuvi Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM). Uamuzi huo mzuri utasaidia kuongeza mapato ya Serikali. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya kutofahamika taarifa mbali mbali muhimu za meli hiyo:

(a) Je, meli hiyo ya uvuvi ina ukubwa gani, *specifications* zake zikoje na utaratibu gani uliotumika kuikodisha kwa KMKM (Je, ukodishaji huo ni wa *time charter*, *bareboat charter* au *voyage charter*).

(b) Je, malipo yake ya kodi ni kiasi gani na yanalipwa kwa utaratibu upi.

(c) Tokea meli hii ilipokabidhiwa kwa Kikosi cha KMKM imezalisha mapato kiasi gani na gharama za uendeshaji ni kiasi gani.

30. MHESHIMIWA ABDULLA HUSSEIN KOMBO (Jimbo la Mkoani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wananchi wengi wa Zanzibar wanaipongeza sana Serikali kupitia Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa kuamua na hatimae kuruhusiwa kufanya biashara ya uvuvi hapa Zanzibar. Hata hivyo, pamoja na kuruhusiwa kufanya biashara hiyo, Kikosi cha KMKM kinalazimika kufuata taratibu za kisheria pale kinapofanya biashara zake.

(a) Je, meli inayotumiwa na Kikosi cha KMKM kuvulia samaki, imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria kufanya kazi hapa Zanzibar.

(b) Je, mabaharia wa meli inayotumiwa na Kikosi hiki, wanazo sifa zinazokubaliwa na kuthibitishwa na mamlaka inayosimamia masuala ya mabaharia wa meli.

(c) Je, mabaharia wa meli hiyo wanafanya kazi kwa kufuata taratibu za kijeshi au taratibu za kiraia.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

37. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Utamaduni wa Mzanzibari ni silaha kubwa katika taifa hili ambalo wananchi wake wanajivunia kuwa na uasili huo unaotokana na sanaa mbali mbali ikiwemo nyimbo za Taarab Asilia. Licha ya hayo, sanaa hiyo imekuwa ikidharauliwa kutokana na kutothaminiwa kwa baadhi ya mambo ambayo ni haiba ya Wazanzibari.

(a) Je, Serikali inaliangalia vipi suala la kuwaenzi wasanii wa Taarab Asilia ambao wameshatangulia mbele ya haki.

(b) Je, Serikali inakuzaje vipaji vya wazawa ambao hawana njia ya kuiga mambo yaliyotokana na sanaa za Taarab Asilia.

(c) Ukiachia mbali malipo yanayotokana na mirahaba, Je Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuandaa matamasha maalumu ya kuwaenzi watunzi na waimbaji wa Taarab Asilia.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

81. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Baadhi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT), zinadaiwa fedha za malipo kutokana na kupatiwa huduma ya umeme katika kuendesha shughuli au kazi za Taasisi hizo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa ndani ya wakati stahiki.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

90. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika barabara ya Wesha Pemba, yapo madaraja pamoja na mipindo mingi tu ambayo inaweza kuleta maafa makubwa, huku kukiwa hakuna alama za barabarani za kuonesha uwepo

wa madaraja na mipindo hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa madaraja na mipindo hiyo kwa hali ilivyo inaweza kusababisha maafa ya ajali kwa wananchi wetu.

(b) Je, ni lini madaraja hayo yatawekewa alama na kuboreshwa zaidi ili kuondoa athari zitakazoweza kujitokeza.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

25. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wananchi, walimu na wanafunzi wa skuli ya Kinowe wanaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwapatia vifaa vya maabara. Hata hivyo, bado ipo changamoto ya nafasi ya kuhifadhia vifaa hivyo.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inalifahamu tatizo hilo.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo.

96. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Msingi ya Kiungoni katika jimbo la Pandani ni miongoni mwa skuli chache duniani zenye mikondo mitatu ya wanafunzi (asubuhi, dhuha na mchana). Ina wanafunzi 1,564; walimu 18 walioajiriwa (badala ya angalau 33 wanaohitajika) na wengi wa kujitolea; vyumba 13 vya kusomea (badala ya 33) na madarasa 33 ya wanafunzi (badala ya 13 tu). Hata hivyo, pamoja na kuwa na upungufu huo wa vyumba 20 vya kusomea na walimu 21 wa kuajiriwa, hakuna hata chumba kimoja cha kusomea kilichoongezeka kama athari ya ahueni ya Uviko-19 isipokuwa kuboresha vyumba vya wananchi ambavyo tayari vilikuwa vinatumika.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa haraka wa kuipatia Skuli ya Msingi ya Kiungoni mahitaji ya lazima ya vyumba vya kusomea, walimu wa kutosha na mahitaji mengine ya msingi kama yanavyoelekezwa na Serikali.

(b) Je, ni utaratibu upi uliotumika katika Skuli ya Msingi ya Kiungoni katika kuibua mahitaji wakati wa kutekeleza mradi wa ahueni ya Uviko 19 na kwa nini Kamati ya Uongozi ya Skuli (SMC) haikushirikishwa.

(c) Kwa vile Skuli ya Msingi ya Kiungoni inakuwa kwa kasi katika kuongeza idadi ya wananfunzi, Je, Serikali haioni haja ya kuwalipa wamiliki wa maeneo yanayokaribiana na Skuli hiyo, ili kuweza kuijengea skuli hii madarasa ya ziada.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

46. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa muda mrefu suala la muingiliano wa majukumu baina ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe Zanzibar, limekuwa likiathiri utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale.

(a) Je, suala hili limefikia hatua gani ya utatuzi wake.

(b) Je, ni changamoto gani Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale inakumbana nazo kutokana na tatizo hilo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

95. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika zeozi la utafutaji wa mafuta na gesi, zipo nyumba na vipando mbali mbali viliathirika na sasa ni muda mrefu bado wamiliki wa nyumba na vipando hivyo hawajalipwa fidia zao.

(a) Je, ni nyumba ngapi ziliathirika na ni lini wamiliki wa nyumba hizo watalipwa fidia zao.

(b) Je, ni watu wangapi waliaoharibiwa vipando au mazao yao.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

133. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Mafuta ya kupikia yasiyo salama hudhorotesha afya ya mlaji na ni chanzo cha maradhi mbali mbali kwa mujibu wa maelekezo ya madaktari wetu.

(a) Je, tuna aina ngapi za mafuta ya kula yaliyo salama kwa matumizi ya kula na kupikia yanayoingia nchini kwetu na kuthibitishwa na 'Zanzibar Bureau of Standards (ZBS)'.

(b) Ni mafuta yepi hayapo salama ambayo Serikali inapendekeza kutokutumika hapa nchini.

**Wizara ya Afya:**

70. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kumekuwa na maonesho pamoja na mafunzo mengi yanayohusiana na matumizi ya dawa za kienyeji maarufu tiba mbadala na kwa kuwa dawa hizo hazina viwango na wananchi wengi wamevutiwa na tiba hii bila kujua na wala kujali athari zake.

(a) Je, ni lini Serikali kupitia Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara ya Afya pamoja na Zanzibar Bureau of Standards (ZBS) watafanya uchunguzi wa kitaalamu ili kuziweka kwenye viwango dawa hizi kwa ajili ya matumizi salama ya binaadamu.

(b) Je, ni lini Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kitaanzisha Kitivo cha Dawa za Kienyeji (Faculty of Traditional Medicines), ili kujenga uweledi kwa wadau wa fani hii katika kutoa huduma kwa wateja wao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Kufuta Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar, Nam. 7 ya 1996 na Kuanzisha Mamlaka ya Mapato Zanzibar kama Chombo Kikuu cha Kufanya Tathmini na Kukusanya Mapato Yaliyoainishwa ili Kusimamia na Kutekeleza Sheria Zinazosimamia Mapato Hayo na Mambo Mengine Yanayohusiana.

Zanzibar,
14 Disemba, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.